Arusha, Tanzania
Website: www.african-court.org
Telephone: +255-27-970-430

**JUDGMENT SUMMARY**

**Conaïde Togla Latondji Akouedenoudje dhidi ya Jamhuri ya Benin**

**Ombi Namba 024/2020**

**HUKUMU KUHUSU SIFA ZA KESI NA FIDIA**

**13 Juni 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

Jijini **Arusha, tarehe 13 Juni 2023**, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya *Conaïde Togla Latondji Akouedenoudje dhidi ya Jamhuri ya Benin.*

Tarehe 4 Agosti 2020, Bwana Conaïde Togla Latondji Akouedenoudje (Mlalamikaji) aliwasilisha Ombi dhidi ya Jamhuri ya Benin (Taifa Lililoshtakiwa).

Mlalamikaji alipinga amri inayohusisha Wizara mbalimbali Namba 023/MJL/DC/SGM/DAPCG/SA/023SGG19 ya tarehe 22 Julai 2019 (amri ya tarehe 22 Julai 2019) inayokataza utoaji wa hati rasmi kwa watu wanaotafutwa na mahakama za Taifa Lililoshtakiwa.

Kwa mujibu wa Mlalamikaji, amri hiyo inakiuka haki zifuatazo: haki ya mshtakiwa kutokuwa na hatia hadi itakapothibitishwa, inayolindwa katika Ibara ya 7(1) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) na haki ya uraia, inayolindwa na Ibara ya 15 ya Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR).

Mlalamikaji aliiomba Mahakama kuamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka haki za binadamu kwa sababu ya Amri ya tarehe 22 Julai 2019 na kumwamuru Mshtakiwa kubadilisha Amri hiyo ili ikubaliane na mahitaji ya kimataifa ya haki za binadamu. Taifa Lililoshtakiwa liliomba Mahakama itangaze kwamba haina mamlaka, kwamba ombi hilo halikubaliki na kwamba Amri hiyo haikukiuka haki ya mshtakiwa kuchukuliwa kuwa hana hatia hadi itakapothibitishwa na haki ya uraia.

Taifa Lililoshtakiwa lilipinga mamlaka ya Mahakama kuwa mwamuzi wa kutoa suluhisho. Mahakama ulitupilia mbali pingamizi hiyo na kuamua kwamba inayo mamlaka ya kuwa mwamuzi wa kutoa suluhisho. Mahakama pia ilichunguza mamlaka yake ya kibinafsi, ya muda na ya eneo. Mahakama iliamua kwamba mamlaka yake ya kusikiliza Ombi hilo yalithibitishwa.

Taifa Lililoshtakiwa liliibua pingamizi kutokana na kutotumia njia zote za ndani za kuleta suluhisho. Mahakama ilitupilia mbali pingamizi hiyo na kuamua kwamba Mlalamikaji alitumia njia zote za ndani za kuleta suluhisho. Mahakama pia ilichunguza mahitaji mengine ya ukubalifu na kupata kwamba yametimizwa. Iliamua kwamba Ombi hili linakubalika.

Kuhusu uhalali, Mlalamikaji alidai kwamba kwa kuamua kutotoa hati rasmi kwa watu wanaotafutwa na mahakama, kwa mujibu wa Amri ya tarehe 22 Julai 2019, hata kama watu hao hawajahukumiwa kuwa na hatia, Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka kanuni ya mshtakiwa kuchukuliwa kuwa hana hatia hadi itakapothibitishwa. Kwa mujibu wa Taifa Lililoshtakiwa, katazo la kutoa hati za mamlaka si utiaji hatia bali linalenga kuzuia watu wanaotafutwa na mahakama kutoroka. Taifa Lililoshtakiwa linaendelea kusema kuwa amri inayohusika inachangia kutetea dhana ya kutokuwa na hatia kiasi kwamba inawaruhusu washtakiwa kufika mahakamani kudhihirisha ama kutokuwa na hatia au kuwa na hatia.

Mahakama ilibaini kuwa mawaziri waliotoa Amri ya tarehe 22 Julai 2019 waliingilia uwezo ambao uko chini ya mamlaka ya mahakama, kwa kuwa hatua za kuzuia ambazo huenda zitekelezwe kwa washukiwa au washtakiwa huamuliwa na, au chini ya udhibiti madhubuti wa, mamlaka ya mahakama. Mahakama ilibainisha kuwa Taifa Lililoshtakiwa halikutoa ushahidi wa notisi au hati yoyote ya kutafutwa iliyotolewa na mahakama, achilia mbali uamuzi wa mahakama unaokataza utoaji wa nyaraka husika kwa watu wanaotafutwa. Mahakama pia ilibainisha kwamba orodha ya watu wanaotafutwa, ambayo inapatikana kwa uwazi kwenye tovuti ya Wizara ya Haki, inajenga hisia ya hatia. Katika kesi hii, Mahakama iliamua kwamba Taifa Llilioshtakiwa lilikiuka Ibara ya 7(1)(b) ya Mkataba.

Mlalamikaji alitoa hoja kwamba haki ya uraia inapaswa kutathminiwa kulingana na ufurahiaji halisi wa manufaa yote ya utaifa, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kufaidika na hati zote za kiraia au kiutawala. Taifa Lililoshtakwa lilisema kwamba amri inayopingwa haihusiani na uraia na haipunguzi uthibitisho wa uraia.

Mahakama iliamua kwamba hatua inayokataza utoaji wa vyeti au inayoamuru ufutaji wake, kama ilivyotungwa na Amri ya tarehe 22 Julai 2019 inaweza kukanusha utu wa kisheria wa watu wanaotafutwa na kusababisha hali sawa na kutokuwa na uraia, ambayo hailingani na lengo linalofuatwa. Mahakama ilipata kwamba Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka haki ya uraia inayolindwa na Ibara ya 5 ya Mkataba ya UDHR.

Mahakama iliamuru Taifa Lililoshtakiwa kufanya kila linalowezekana kubatilisha Amri inayohusisha Wizara mbalimbali ya tarehe 22 Julai 2019.

Mahakama iliamua kwamba kila mdaawa atajilipia gharama zake.

Jaji Blaise TCHIKAYA alitoa maoni tofauti ambayo yameambatishwa kwenye hukumu kwa mujibu wa Ibara ya (7) ya Mkataba na Kanuni ya 70(1) ya Kanuni za Mahakama.

**Taarifa zaidi**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na matini kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inapatikana katika *https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0242020*

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Masijala kwa barua pepe kupitia registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha kuna ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka juu ya kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusu ufasiri na matumizi ya Mkataba, Protokali hii na hati zingine zozote za Haki za binadamu zilizoidhinishwa na Mataifa husika. Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*